

**JUA  
HAKI  
ZAKO**

**UHAMIAJI**

**JUA  
HAKI  
ZAKO**



**ACLU** Kentucky

[aclu-ky.org](http://aclu-ky.org)

[@acluofky](https://twitter.com/acluofky)



## **JINSI YA KUPUNGUZA HATARI KWAKO MWENYEWWE**

- Tuliza nafsi. Usipinge wala kuzuia maafisa au mawakala.
- Usiseme uongo wala kutoa nyaraka za kughushi.
- Jiandae wewe na familia yako iwapo utakamatwa.  
Kumbuka nambari za simu za familia yako na wakili wako. Tengeneza mipango ya dharura ikiwa una watoto au unatumia dawa.

## **IWAPO UTAKUTANA NA MAWAKALA WA ICE KAZINI**

- Uliza kama uko huru kuondoka. Ikiwa ndivyo, ondoka kwa utulivu.
- Una haki ya kukataa ruhusa ya kukaguliwa.
- Una haki ya kunyamaza. Huna haja ya kujadili hali yako ya uhamiaji na mtu yeyote, kama vile mahali ulipozaliwa, kama wewe ni raia, au jinsi ulivyoingia nchini.
- Ikiwa una nyaraka halali za uhamiaji, unapaswa kuzionyesha. Kamwe usitoe nyaraka za kughushi.
- Ukikamatwa, sema kuwa unataka kunyamaza hadi uongee na wakili.
- Una haki ya kurekodi mazungumzo yako na maafisa wa uhamiaji alimradi hautatizi.

## **IWAPO MAAFISA WA ICE WATATOKEA MLANGONI KWAKO**

- Huna haja ya kufungua mlango. Ukifungua, tulia - una haki zako.
- Uliza wamefika kwa sababu gani (na uombe mkalimani ikiwa unamhitaji).
- Wakikuomba kuingia, waulize kama wana hati ya upekuzi iliyosainiwa na jaji na kama ipo, iombe uione (kupitia dirishani au wasukume chini ya mlango).
- Kama hawana hati ya upekuzi iliyosainiwa na jaji, unaweza kukataa kuwapa ruhusa ya kuingia. Waombe waache taarifa yoyote mlangoni.
- Wakilazimisha kuingia, usipinge. Waambie wote waliopo ndani wabaki kimya.
- Ukikamatwa, una haki ya kunyamaza. Usisaini kitu chochote kabla ya kuzungumza na wakili.

## **NINI CHA KUFANYA UKIKAMATWA AU KUZUILIWA**

- Una haki ya kuwasiliana na ubalozi wako au kuomba afisa awaarifu kuhusu kuzuiliwa kwako.
- Kumbuka nambari yako ya uhamiaji ("A" number) na uipe familia yako. Itawasaidia kukupata.